

WAEBRANIA, MLANGO WA KWANZA



Na kutoa ninii ki—kidogo. . . Nafikiri hakuna kitu kilicho kizuri zaidi, kwangu mimi, kuliko Neno peke yake. “Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu.”

² Siku za Jumatano, na labda siku za Jumapili, moja ya ibada za Jumapili, kumpa mchungaji mapumziko mafupi kidogo, jambo ambalo analistahili, basi nilifikiri labda tungechukua tu Kitabu kimoja katika Biblia. Tulikuwa na mazoea ya kufanya jambo hilo, na wakati mwingine tunakaa mwaka mzima kwenye jambo hilo.

³ Ninakumbuka wakati mmoja tulikaa mwaka mzima mfululizo kwenye Kitabu cha Ufunuo. Lakini, loo, jamani, ni ajabu mambo tuliyojifunza, na jinsi gani vile yalivyokuwa ni ya kustaaajabisha! Kisha tukarudi nyuma na kuchukua Kitabu cha Danieli, ama Kitabu cha Mwanzo, ama Kutoka, na kukipitia tu, mlango kwa mlango, na kiliunganisha tu Biblia nzima pamoja. Loo, kwa kweli ninapenda jambo hilo!

⁴ Baadaye kidogo, itatubidi tupate ninii. . . Kama Bwana akiendelea kubariki nasi tuendeleo, tutaingia kwenye baadhi ya mambo ya kilindi sana hapa, ya kilindi hasa. Nasi tutaenda toka mahali hadi mahali, kupitia kwenye Maandiko, pamoja na mambo hayo.

⁵ Nami ninapenda kufanya Andiko lilinganishwe na Andiko. Hivyo ndivyo jinsi inavyopaswa kuwa. Ni picha moja kubwa nzuri sana tu. Na katika kitabu hiki tunachojifunza, tutaingia, loo, wokovu, na uponyaji wa Kiungu, na miujiza, na rehema nyingi. Na, loo, kila kitu kinaingia hapa.

⁶ Na huenda nitakapofikia mahali ambapo itanibidi kwenda kwenye mikutano. . . kamwe sijui wakati gani nitakapokuwa hasa kwenye mkutano, kuitwa kwenye mkutano, kwa kuwa sina kitu chochote kilichopangwa mpaka ninapojisikia kabisa kuongozwa kufanya jambo fulani. Na hilo pengine likawa ni kabla ya asubuhi, huenda nikaruka kwa ndege kwenda California, mpaka Maine ama mahali fulani, mahali popote tu ambapo angeniita. Hiyo ndiyo sababu sijipangii milolongo mikubwa na mirefu ya safari, kwa maana siwezi kufanya hivyo. Huduma yangu haina mpangilio wa namna hiyo, na iko tofauti tu.

⁷ Na sasa nimekuja nyumbani kwa mapumziko mafupi tu. Nimepungua ratili ishirini, katika mkutano huu wa mwisho. Na

Ndugu Mercier na Ndugu Goad walikuwako kule, muda mfupi uliopita, nao wakasema, “Ndugu Branham, ninaona unayofanya. Unaweka moyo wako wote katika hiyo.”

⁸ Nikasema, “Hivyo ndivyo jinsi pekee unavyoweza kufanya namna ya kazi nzuri kwa ajili ya Bwana, ni kuweka kila kitu ulicho nacho mstari wa mbele kabisa kwa ajili ya Kristo; nguvu zako zote, nafsi yako yote, moyo wako wote, akili zako zote, kila kitu ulicho nacho.” Unapokuwa ukifanya jambo lolote, lifanye sawasawa la sivyo usilifanye kabisa, unaona, hebu liache tu lilivyo. Kama utakuwa Mkristo, weka kila kitu ulicho nacho kwa Kristo, hiyo ni kusema, muda wako, kipaji chako, kila ulicho nacho.

⁹ Sasa hivi tu ndio ninamwona huyu kijana. Huyu ni mke wako, Ndugu Burns, sivyo, anayepiga kinanda na kuimba pale, hao maharusi vijana. Na—na si piano, wala kinanda, bali ni namna fulani ya ala, wanakipigapiga na kukidonoa, na kufanya jambo fulani kwa ajili ya Bwana. Kama ungaliweza kufanya hivyo, na kuimba, hiyo ni kusema, kuvuta nafsi. Fanya jambo fulani, haidhuru. Kama u—unaweza kupiga mbinja, vema, piga mbinja. Hebu fanya jambo fulani tu. Hebu shuhudia tu ama fanya jambo fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Chochote ulicho nacho, kitumie katika utumishi wa Mungu.

¹⁰ Sasa, hatutathubutu kutaka kukaa kirefu sana, kwa kuwa ninajua ninyi mnafanya kazi. Inawalazimu kuamka mapema. Nami ninaenda kuwinda kindi kila asubuhi. Nitawaambia tu ukweli. Hicho ndicho ninachofanya. Hicho ndicho kilichonifanya nije nyumbani, ni kupumzika kidogo. Na kwa hiyo ninaamka, yapata saa kumi, na kutoka kuingia msituni na, vema, kuwinda kidogo kisha ninaingia usingizini. Nami ninarejesha kiasi fulani cha ule uzito, kwa hiyo nitajipumzisha, baada ya kitambo kidogo, kama ninyi. . .Bwana akipenda. Na kila kitu kiko sawa.

¹¹ Vema, sasa, tutafungua katika Biblia zenu. Ninawataka mlete Biblia zenu kila usiku, ambazo mnaninii. . .kama mwezavyo. Kama mtu anakosa chache, kama mtu akitaka kufuatilia usomaji, tuna chache hapa, tungekuwa na ninii. . . baadhi ya mabawabu kuzipitisha. Kuna mtu anayetaka moja? Vema, inua tu mkono wako.

¹² Sijui kama Ndugu. . .Doc, njoo hapa uchukue Biblia hizi. Umesimama hapo karibu, na Ndugu Burns. Hilo ni sawa, Burns? Nilimsikia akisema. . .[Ndugu huyo anasema, “Conrad.”—Mh.] Ati nini? [“Conrad.”] Conrad. Nilimwita. . .Kidogo ninapata shida ya kusikia, labda, Ndugu Neville. Nilipataje jina la Burns? Ninamjua mtu huyo kwa sura, nami siwezi tu, sikuweza kulikumbuka jina lake.

¹³ Nanyi mnajua, unapozidi kuzeeka kidogo zaidi, ninaona jambo moja, ni vigumu zaidi kwangu kusoma Biblia hii. Nami

ninachukia tu kuwazia jambo la kulazimika kuvaa miwani, kusoma Biblia.

14 Lakini, hapa si zamani sana, nilidhani nilikuwa ninakuwa kipofu. Ndipo nikatoka kwenda kumwona Sam. Ndipo Sam akasema, “Bill, sijui.” Kasema, “Nitakufanyia tu miadi na mtaalamu fulani.”

15 Nikaenda Louisville. Hapana budi yalikuwa ni mapenzi ya Bwana. Bingwa fulani mashuhuri; ninasahau jina lake sasa. Lakini alikuwa amesoma kitabu changu. Naye akasema, “Kama wakati wowote utarudi Afrika, ninataka kwenda na wewe.” Akasema, “Na kama ukininii. . . Hao Waafrika wanakupenda.” Kisha akasema, “Wao ni washirikina sana, hasa sana kwa swala la kisu, kufanyiwa upasuaji. Kwa hiyo,” kasema, “Ninataka kutoa miezi sita ya maisha yangu, kwa ajili ya upasuaji wa watoto wa macho na kadhalika, kwenye ninii. . . kwenye umisheni.” Tena akasema, “Kama tungeweza kwenda pamoja, nawe ungeweza kupata kibali kwao, namna hiyo.” Kasema, “Basi kama walikuwa na watoto wa macho na shughuli za macho,” kasema, “ningependa sana kulifanya hilo, bila malipo, miezi sita kwa kazi hizo.” Nami ninasahau inabidi mtu kungoja muda gani upate miadi naye.

16 Nasi tulikuwa tumeketi kwenye chumba kidogo nacho kilikuwa na nuru ndogo—ndogo nyekundu iliyowashwa, huko nyuma kwenye hicho chumba chenye giza. Mbona, niliweza kusoma herufi hizo. Ilisema ishirini-ishirini. Niliweza kuzisoma kwa namna mojawapo. Ndipo akaiweka kwenye kumi na tano-kumi na tano, nami niliweza kuzisoma. Kisha akaiweka kwenye kumi-kumi, nami niliweza kuzisoma. Akasema, “Vema, macho yako hayana shida kubwa.”

17 Kwa hiyo alikuwa na darubini ndogo. Akaweka kidude kidogo kule nyuma, kitu kidogo, unajua. Zile darubini za kale, ni wangapi wanaozikumbuka? Tulikuwa tukizitumia, kuangalia picha, namna hiyo tu. Ndipo akasema, “Je! Unaweza kusoma hayo?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Nisomee.”

18 Ilikuwa na, loo, aya nzima, karibu namna *hiyo*. Nikaanza, kuisoma; akaanza kuivuta juu, namna *hiyo*, nikizidi kupungua kasi nikisoma pole pole. Akafikia mahali kama *hapa*, nikakoma. Akasema, “Ninaweza kukwambia jambo moja, umepita umri wa miaka arobaini.”

Nikasema, “Naam, hiyo ni kweli, niliupita zamani.”

19 Akasema, “Umemudu namna gani?” Akasema, “Jicho la binadamu, kwa maumbile ya kawaida, unapofikia umri wa miaka arobaini, kama vile nywele zako zinavyoingia mvi, na kadhalika, mboni ya jicho inakuwa bapa.” Kasema, “Sasa,

kama ukiishi muda mrefu vya kutosha, hali yake ya kawaida itarudi tena.” Akasema, “Huo ni uwezo wa pili wa kuona, ndivyo wanavyouita. Bali,” kasema, “binadamu, mwenye umri wa miaka kama arobaini, kwa kweli wataninii. . .” Kasema, “Macho yao hayana kasoro.”

20 Ninaweza—ninaweza kuona unywele kama ungalikuwa sakafuni, niutoe kwangu. Lakini ukinikaribia. . . Naye akasema, “Sasa, ukiisoma Biblia yako,” kasema, “unaisogeza mbali kutoka kwako.” Kasema, “Baada ya kitambo kidogo, mkono wako hautakuwa mrefu vya kutosha, mpaka huwezi—huwezi kuiweka huko mbali vya kutosha kuweza kuishika.”

21 Na kwa hiyo akanitengenezea miwani moja, na sehemu ya chini unaweza, ni ya kusomea. Akasema, “Sasa, kwenye mimbara yako. . .” Alidhani mimi ni mmojawapo wa hawa hapa wahubiri waheshimiwa, unajua. Na kwa hiyo akasema ya kwamba ninii. . . wewe. . . Sehemu ya juu ni kioo tu cha kawaida cha dirisha, kioo cha kawaida tu. Na sehemu ya chini ina namna fulani ya kukereza, hivi kwamba ninaweza kusoma kwa karibu, unajua, namna *hiyo*. Kwa hiyo ninachukia tu kuivaa; ninachukia.

22 Na sasa, katika mafundisho ya Biblia, nami nina Agano Jipya usiku wa leo. Kwa hiyo ni ninii. . . Nina Agano Jipya la Collins. Lina maandishi makubwa vya kutosha. Lakini sasa, nikirejea kwenye ile nyingine, huenda ni—nikavichukua hivyo vipenzi vyangu vya zamani, na—na kwa namna fulani kusoma kupitia hivyo. Lakini haidhuru ni nini, ni—nina furaha ya kwamba bado nina kitu fulani ni—ninachoweza kusoma. Na—na—na chochote nilicho nacho, nitaenda kumpa kila mtu chochote niwezacho, kwa utukufu wa Mungu, natumaini ya kwamba ataondolea mbali dalili hiyo ya uzee. Siwezi kumwomba aniondolee mbali umri wangu. Mimi. . . Mwajua, hilo ndilo jambo moja tu linalotubidi sote kutupata. Inabidi tupitie huo. Nami ninajua mimi si mvulana mdogo kama vile nilivyokuwa sikuzote, nikisimama hapa jukwaani. Nina umri wa miaka arobaini na minane. Na hebu wazieni tu, miaka miwili zaidi, nitakuwa na umri wa miaka hamsini, Ndugu Mike.

23 Jamani, ni vigumu kwangu kuamini hilo! Ninaninii tu. . . Sikujuu kamwe kwamba nilikuwa nimepita umri wa miaka ishirini mpaka yapata miaka miwili iliyopita. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ninaninii tu. . . Sikuweza kuamini jambo hilo. Na hata hivyo ni—ni. . . Ni vigumu kwangu kuamini mpaka nilipoangalia kwenye kioo, na ndipo ni—ninajua ndivyo ilivyo, basi. Lakini—lakini kuwa tu nikiangalia, ninajisikia tu vizuri tu kama nilivyowahi kujisikia maishani mwangu, nami ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo, pia. Sifa zote apewe Mungu.

24 Sasa, tunajifunza Kitabu cha Waebrania. Kimekuwa . . . Loo, ni kimoja cha Vitabu vyenye kilindi sana, tajiri sana vya Biblia. Ninawaambia, ni Kitabu ambacho kweli kitaninii . . . Mungu akiruhusu, na tukiingilie, ninaamini tutapata uhondo mtamu sana hata tutapiga makelele ya kumsifu Mungu daima. Na sasa mimi . . .

25 Kitabu cha Waebrania, kwa kweli vile kilivyo ni kwamba, kinadhaniwa kiliandikwa na Mtakatifu Paulo, yule mfafanuzi mkuu sana wa Biblia, nadhani, ambaye ulimwengu ulipata kuwa naye, isipokuwa Bwana wetu Yesu Kristo. Na Paulo alikuwa akitenganisha ninii . . . Sasa, Paulo alikuwa ni mwalimu halisi wa Biblia; hiyo ni kusema, Agano la Kale. Hicho ndicho Kitabu pekee kilichokuwa kimeandikwa wakati huo, kilichoitwa Biblia. Naye alikuwa akijaribu kuwaonyesha Waebrania, akitenganisha Agano la Kale na kuonyesha Agano la Kale kuwa ni kivuli ama mfano wa lile Jipya.

26 Papo hapo tungeweza kugusa jambo muhimu kabisa na tukae miezi mitatu papo hapo kwenye wazo hilo moja, papo hapo. Kurejea moja kwa moja nyuma, kama tungeweza kufungua kwenye Biblia zetu sasa, bila shaka tuko kwenye Waebrania, mlango wa 1. Lakini kama tungefungua kwenye Ufunuo, mlango wa 12, ungeweza kuona jambo hilo kikamilifu tena, jinsi ilivyo hivyo vivuli. Kama . . . ninyi mlio na penseli zenu na mtakaoyaandika Maandiko. Katika Waeb- . . .

27 Katika Ufunuo 11, tunaona ya kwamba Yohana, kwenye kisiwa cha Patimo, alimwona mwanamke amesimama mbinguni, naye alikuwa amevikwa jua kichwani mwake na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake. Naye mwanamke huyo alikuwa katika utungu wa kuzaa, akiwa na mimba. Akamzaa mtoto mwanamume. Lile joka jekundu lilisimama, lipate kumla mtoto huyo mara atakapozaliwa. Ndipo yule—yule mtoto akanyakuliwa hadi Mbinguni, naye huyo mwanamke akakimbilia nyikani ambako alilishwa kwa wakati, wakati, na nusu wakati, ama katikati ya wakati.

28 Sasa, huyo mwanamke aliwakilisha kanisa, na huyo Mtoto ambaye alimzaa alikuwa ni Kristo. Ule mwezi chini ya miguu yake ulikuwa ni torati, jua kichwani pake lilikuwa ni neema. Nyota kumi na mbili kwenye taji lake zilikuwa ni wale mitume kumi na wawili. Na hapo ndipo ambapo, kwenye ninii . . . Wale mitume kumi na wawili walikuwa ni utukufu ama kutiwa taji kwa Agano Jipya. Unaona? “Kwa maana hakuna misingi mingine inayoweza kuwekwa kuliko ile iliyokwisha kuwekwa.” Unaona? Huo, ule Msingi, A—Agano Jipya, wale mitume, Fundisho la mitume, na kadhalika, ndiyo taji ya msingi wa Agano Jipya. Na halafu kwenye ninii . . .

29 Mwezi ni kivuli cha jua. Jua huakisi tu nuru yake linapokuwa nyuma ya dunia. Nao mwezi hutoa nuru, ya kutembelea, usiku.

Na ni picha nzuri jinsi gani tuliyo nayo hapa, picha nyingine nzuri: jua linamwakilisha Kristo; mwe—mwezi unaliwakilisha Kanisa. Wao ni kama tu mume na mke. Na Kristo asipokuwapo, Kanisa linaakisi Nuru ndogo, Injili. Na ni—ni Nuru ya kutembelea mpaka Mwana atakapotokeza tena, ndipo Kanisa na Mwana, mwezi na jua, vitaungana pamoja. Unaona? Mwezi ni sehemu ya jua, na Kanisa ni sehemu ya Kristo. Na wakati Kristo hayupo, Kanisa huakisi Nuru Yake. Na kwa hiyo hakika tu jinsi tunavyoweza kuona mwezi ukiwaka, huo unajua jua linawaka mahali fulani. Na mradi Kanisa linaakisi Nuru ya Kristo, Kristo yuko hai mahali fulani. Amina. Wazia jambo hilo.

³⁰ Sasa, torati ilikuwa ni mfano wa neema, lakini torati haikuwa na nguvu za kuokoa ndani yake. Torati ilikuwa ni ninii tu. . . Torati ilikuwa ni polisi. Polisi alikutia jela, bali, unaona, ilihitaji neema kukutoa gerezani. Unaona?

³¹ Kwa hiyo Damu ya Kristo, Injili, hutukomboha na dhambi. Torati hutufanya tu wenye dhambi. Torati ilisema tu, “Wewe ni mwenye dhambi. Usiibe. Usizini. Usishuhudie uongo.” Unaona? Ni polisi anayesema wewe umekosa na una hatia. Lakini Injili ni habari njema. Kristo alikufa atuokoe na makosa yetu yote, uvunjaji wa sheria. Kristo alikufa apate kututoa.

³² Sasa, Paulo, mara alipoongolewa, hakushauriana kamwe na seminari yoyote, wala hakuwataka shauri wahudumu wowote. Lakini je, hivi ulifahamu? Alishuka akaenda Arabuni, naye alikuwa huko miaka mitatu, huko Arabuni. Sasa, hii ni, nionavyo mimi, ile. . .

³³ Sasa, hatuna budi kupata msingi wa jambo hili, ili kwamba tujue jinsi lilivyo tajiri. Na somo la kwanza, usiku wa leo, tutachukua msingi wetu.

³⁴ Sasa, Paulo alikuwa mwalimu wa Biblia wa jinsi hiyo, kwa maana alifundishwa chini ya yule mtu mkuu Gamalieli, aliyekuwa bora kuliko wote wakati ule. Naye alikuwa mmoja wa watu mashuhuri sana wa kizazi chake, yule mwalimu mkuu wa torati na manabii. Kwa hiyo, Paulo alikuwa amefunzwa vizuri sana katika mambo hayo.

³⁵ Na halafu mimi ninampenda kwa namna hii, ufunuo huu mkuu, akiwa mwaminifu moyoni mwake, mwaaji, alikubaliana na kifo cha Stefano naye akamwona Stefano akifa kwa kupigwa mawe na kupigwa mabonge ya mawe hata akafa. Hapana shaka nafikiri lilimgusa Paulo sana wakati alipomwona Stefano akiinua mikono yake Mbinguni, na kusema, “Ninaona Mbingu zimefunguka. Ninamwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu.” Ndipo akasema, “Baba, usiwahesabie dhambi hii.” Ndipo akalala mauti.

³⁶ Je! uliona jambo hilo? Yeye kamwe hakufa. Alilala mauti. Kama vile tu. . . Siamini kwamba kamwe alisikia jiwe lingine

hata kidogo. Ni kama tu mtoto mchanga kifuani mwa mama yake, anavyolala, Stefano alilala mauti mikononi mwa Mungu.

³⁷ Kuna kitu fulani, kumhusu Paulo, kilichomkera. Ndipo yeye, mtu yeyote chini ya uhakika kabisa, akijaribu kulipiga vita, anaenda kwa kuhani mkuu na kupata nyaraka fulani. Kasema, “Nitawaweka mbaroni hao watu wote wanaopiga makelele hayo yote, na hao wazushi;” walidhaniwa, vile tungeita siku hizi, baadhi ya “walokole wenye siasa kali,” ama kitu fulani kama hicho, wanaopiga makelele sana na kusababisha vurugu. “Tutashuka twende tukalimalize jambo hilo.”

³⁸ Ndipo alipokuwa akienda zake njiani, kijininii cha zamani. . . si njia kuu kama tunayosafiria. Na barabara hizo huko Palestina, vijinjia vidogo tu, kama njia ya ng’ombe inayopitia mwituni ambapo ng’ombe, na kondoo, na farasi, na punda, na ngamia, walipanda kwenda vilimani.

³⁹ Ndipo Paulo, akiwa njiani kwenda Dameski, yapata aduhuri, siku moja, Nuru kuu ikimwangazia na ikamwangusha chini. Hakuna mtu aliyeiona ila Paulo. Ninawatakeni mwone jambo hilo. Na papa hapa, hili si la kibinafsi sasa, bali ni ili kwamba tuelekee kwenye msingi huu. Mpate kujua jambo hilo ya kwamba Yesu huyo huyo. . .

⁴⁰ Sasa, wakati alipokuwa hapa duniani, alisema, “Nilitoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu.”

⁴¹ Sasa, wakati alipowaongoza wana wa Israeli, Yeye alikuwa Nguzo ya Moto. Naye alikuwa amefanyika mwili, kisha akarudi kwenye Nguzo ile ile ya Moto. Na wakati alipokutana na Paulo akiwa njiani kwenda Dameski, Yeye alikuwa ni ile Nguzo ya Moto, ile Nuru, unaona, Nuru kuu. Ndipo Paulo akasema, “Ni nani Huyo ninayemwuudhi?”

⁴² Akasema, “Mimi ni Yesu, unayeniudhi,” ile Nuru. Loo, Yeye si ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁴³ Na Huyu hapa, usiku wa leo, papa hapa pamoja nasi. Alipigwa picha Yake moja kwa moja pale, Jambo lile lile, unaona, Nguzo ya Moto, Nuru, jinsi vile vile tu kama Yeye alivyokuwa, “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁴⁴ Sasa wale watu waliokuwa pamoja naye hawakuiona ile Nuru, bali ilikuwapo pale hata hivyo. Matokeo yalionyesha jambo lile lile.

⁴⁵ Sasa, je! inawezekana ya kwamba—ya kwamba mtu fulani angeweza kumwona Kristo katika jengo hili na wala mtu mwingine yeyote asimwone? Hakika. Lilitendeka pale.

⁴⁶ Ilitukia pia usiku mmoja wakati Petro alipokuwa gerezani. Na Nuru hiyo iliingia mle gerezani, na kumgusa Petro, naye akatembea moja kwa moja karibu na mlinzi wa ndani, mlinzi wa nje, akatembea karibu na lango, lango kuu, kisha kwenye lango la mji. Petro akasema, “Hapana shaka nilikuwa nikiota ndoto.”

Lakini aliangalia kote kote, lakini ile Nuru ilikuwa imeondoka; Kristo, yule Nuru ya Milele, ya daima. Huyu *hapo*. Sasa, akiwa njiani akienda . . .

⁴⁷ Basi angalia, jambo lingine, kama tungezungumzia jambo hili, ndio kwanza liingie mawazoni mwangu. Lakini wale mamajusi walioifuata ile Nyota, njia nzima kutoka India, pande za Mashariki, miezi, wakipitia mabondeni na kwenye majangwa, ilipita juu ya vituo vya utafiti. Nao walishika majira ya saa za usiku kwa kuangalia nyota. Wala hakuna mwanahistoria wala yeyote yule aliyepata kutajwa aliyewahi kuiona hiyo Nyota ila wale mamajusi. Ndio pekee waliokusudiwa kuiona.

⁴⁸ Kwa hiyo unaweza ukaona vitu ambavyo huyo jamaa mwingine huenda asivione. Kwako, ni jambo halisi. Kwake, wao hawaelewi. Ni kama tu kuongoka; unaweza kuongoka na kufurahia baraka za Mungu, uki—ukinywa tu baraka za Mungu. Na jamaa huyo mwingine, akiketi karibu na wewe, “Sioni kitu.” Unaona? Unaona? Hivyo ndivyo ilivyo. “Siwezi tu kulielewa. Sioni yote hayo yana maana gani.” Vema, yeye halielewi tu. Hivyo tu. Ambapo, wewe unalifahamu.

⁴⁹ Angalia sasa, Paulo akishuka kwenda zake. Na mara tu tukio hili kuu lilipompata . . . Sasa, yeye hakuridhika . . . Hilo ndilo linalomfanya Paulo kuwa wa kuaminika sana, sasa.

⁵⁰ Somo letu usiku wa leo halina kilindi. Ni somo la juu juu, lakini, loo, tutaingia kwenye kilindi, muda si muda. Lakini hili ni somo rahisi sana, bali linaanza tu. Na jambo ni kwamba, ni jambo moja, hilo ni kumtukuza Yesu Kristo. Paulo, anapoanza.

⁵¹ Na kabla hajafanya jambo hili, Paulo alikuwa ni mwanafunzi wa Biblia. Na mwanafunzi wa Biblia kamwe hataweka fundisho lake juu ya uzoefu wa mambo. La, bwana. Kamwe hawataweka fundisho lao kwenye tukio wa mambo fulani. Unaweza kupata ujuzi wa namna yoyote. Lakini halina budi kuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Kabisa.

⁵² Sasa, katika Agano la Kale, walikuwa na njia tatu mbalimbali wanazoweza kuhakikisha ujumbe. Kwanza, torati, hiyo ilikuwa tu ni torati. Halafu, walikuwa na na—nabii; mwotaji; kisha walikuwa na Urimu Thumimu. Sasa hilo linaweza kuwa ni la kilindi kidogo.

⁵³ Urimu Thumimu ulikuwa ni kifuko cha kifuani ambacho Haruni alivaa kifuani mwake. Kwenye hicho kulikuwa na mawe kumi na mawili: yaspi, akiki, baharamani, na kadhalika, na kuendelea. Walichukua mawe yote kumi na mawili makubwa, yaliyokuwa kwenye kifuko cha kifuani, ikionyesha ya kwamba alikuwa ni kuhani mkuu wa kila kabila, yale makabila kumi na mawili ya Israeli. Kifuko hiki cha kifuani kilining’inia kwenye nguzo kanisani. Ndipo nabii alipotabiri, nao walitaka kuhakikisha jambo hilo lilikuwa ni kweli, ama si kweli, manabii hao ama waotaji hao walisimama mbele ya Urimu Thumimu hii,

naye akasimulia ndoto yake ama ono lake, chochote alichokuwa ameonaa. Na kama hiyo Nuru Takatifu. . . Loo, unaona jambo hilo? Mungu daima aliishi katika ulimwengu wa kiroho. Kule kuchanganyika pamoja, zile nuru, zilikuwa ni za kawaida tu mpaka sauti hii iliposimulia. Basi wakati hiyo sauti ilipoyagusa mawe yale, kama haikuwa ni ya kimbinguni, hayakufanya kitu. Bali kama ilikuwa ni ya kimbinguni, hizo Nuru zote kwa pamoja ziliakisi rangi ya upinde wa mvua. Amina. Basi, huyo alikuwa ni Mungu akinena, “Huyo ni nabii Wangu. Hiyo ndoto ilitoka Kwangu.” Walipambanua kulingana na Urimu Thumimu.

54 Je! unakumbuka Sauli wakati aliporudi nyuma? Alisema hakuweza kupata ndoto. Naye yule nabii, Samweli, alikuwa amekufa, wala hapakuwa na jinsi yoyote ile. Akasema, “Hata Urimu haunizungumzii.” Hakuna chochote. Sauli alisimama mbele ya Urimu, na maneno yake yalikuwa ni mshindo wa sauti zilizokufa. Unaona? Mungu alimkataa kabisa. Na hizo Urimu Thumimu, hilo lilikuwa ni thibitisho la Haruni la ukuhani wake. Baada ya Haruni kuondoka, Musa. . . Ki—kisahani hicho kilining’inizwa kwenye nguzo.

55 Sasa. Ukuhani wa Haruni ulikoma wakati Yesu alipokufa. Na sasa, hilo lilitenganisha torati na neema, nasi tungali tuna Urimu Thumimu. Na Paulo alikuwa akizitumia. Unaona? Urimu Thumimu siku hizi ni Neno la Mungu Lisilopatikana na Mauti, la Milele, la daima. Unaona?

56 “Kwa maana yeyote atakayeondoa lolote toka kwenye Kitabu hiki, ama kuongeza chochote Kwake.” Sitaki kitu chochote nje Yake, bali ninataka yote kilicho nayo. Hilo ndilo Kanisa tunalotaka. Na mambo yote hayana budi kuthibitishwa kwa Neno.

57 Hiyo ndiyo sababu nilipingwa sana na Wapentekoste hivi majuzi, kwa sababu, ya kusema, “Nisingeweza kuelewa ambapo mafuta yakitoka mikononi mwako, ama damu kutoka usoni mwako, ilikuwa ni ishara wewe ulimpata Roho Mtakatifu.” Hilo si la Kimaandiko wala ni—nisingelikubali. Halina budi kutoka kwenye Neno.

58 Na sasa, Paulo, yeye alipenda tu Neno. Kwa hiyo, kabla hajashuhudia tukio hili kuu alilokuwa nalo, alishuka akaenda Misri kwa miaka mitatu. Ninaamini ilikuwa ni miaka mitatu, miaka mitatu huko Misri. Na mnajua ninachoamini yeye alifanya? Ninaamini ya kwamba alichukua Agano la Kale, na akachunguza katika Agano la Kale lote, naye akakuta kwamba Huyu alikuwa kweli ndiye huyo Masihi halisi. Ilibidi athibitishwa tukio lake kwa Biblia. Amina. Loo, jamani!

59 Mwangalie wakati alipokuwa gerezani. Unaona, kuna ki—kipindi cha maisha ya Paulo wakati alipokuwa gerezani kule kwa muda mrefu. Yeye aliandika Kitabu cha Waefeso. Aliandika Waraka huu wa Waebrania. Unaona? Alikuwa na wakati. Mungu

alimweka huko gerezani, na akaandika Nyaraka hizi kwa makanisa. Mmoja kwa kanisa la Efeso. Aliandika mmoja kwa kanisa la Kipentekoste, alipata shida nyingi sana nao. Kanisa hilo la Kipentekoste alikuwa na shida zaidi nalo kuliko mtu mwingine yeyote. Angali ana shida nalo. Bali alishukuru kwa ajili yao. Jambo pekee aliloweza kuwafundisha. . . Walipoingia: mmoja alikuwa na lugha, mmoja alikuwa na zaburi, mmoja alikuwa na mhemuko, mmoja alikuwa na hisia. Asingeweza kuzungumza, kusema nao, “Usalama wa Milele.” Asingeweza kuwazungumzia, “kuchaguliwa tangu zamani.” Asingeweza kuwazungumzia wa. . . Walikuwa ni watoto wachanga. Wote ilibidi wa—wahisi kitu fulani, ama waone kitu fulani, ama wawe na hisia za ajabu ajabu, na, ama wawe na kitu fulani karibu yao, thibitisho fulani.

⁶⁰ Bali ninaamini, alipozungumza na Waefeso, angeweza kuzungumza juu ya “Mungu ametuchagua tuwe wana na binti, na kutufanya wana katika Kristo Yesu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Hebu angalia jambo hilo. Jamani!

⁶¹ Mwangalie akija kwenye Kitabu cha Warumi, na kadhalika. Walikuwa watu wazima. Loo, walinena kwa lugha, hakika, na walikuwa na ishara nyingine za Roho Mtakatifu miongoni mwao. Lakini hawakufanya mafundisho, na mihemuko, na kutetemeka kudogo, na hisia za ajabu.

⁶² Paulo alisema, “Mna—mna—mnavuka mpaka katika mambo hayo. Wakati mnapaswa kuwa mnafundisha, mngali mu watoto wachanga na inawabidi kunywa maziwa.”

⁶³ Hilo ndilo daima nililojaribu kushindania kutoka maskani hii iwe hivyo, si kundi la watoto wachanga. Hebu na tuwe watu wazima. Tusimame barabarani. Loo, jamani! Unaona.

⁶⁴ Kwa hiyo, Paulo anashuka anaenda kule, kwanza, kuona kama tukio lake lililingana na Biblia ya Mungu.

⁶⁵ Loo, je! lisingekuwa ni jambo zuri sana, siku hizi, kama watu tu wangelifanya tu jambo hilo tena, kama tungalilinganisha tukio letu na Biblia ya Mungu? Kama halilingani, basi tukio letu ni la makosa; halimuliki kwenye Urimu Thumimu. Kama linamulika Humo, amina, tumempata. Lakini kama haumuliki, baadhi. . . sijali linaonekana ni zuri jinsi gani, jinsi lilivyoonekana halisi la kweli; kama nuru hizo hazikumulika kwenye Urimu Thumimu hizo, jambo hilo lilikuwa ni makosa.

⁶⁶ Na haidhuru wewe umekuwa na tukio la namna gani, jinsi tukio hilo linavyoonekana kuwa halisi, jinsi lilivyo la kuvutia, jinsi lilivyo la kielimu, kwamba ni chombo kikuu jinsi gani cha kuvuta nafsi; kama halimuliki katika Neno, ni la makosa. Kweli. Halina budi kupatana na Neno.

⁶⁷ Sasa, ninaamini, na kuna njia ya katikati. Barabara, sasa, mara nyingi. . . Nilikuwa nikihudhuria kanisa fulani la

Wanazarayo. Bwana na awabariki watu hao wapendwa. Wao ni Wamethodisti wa mtindo wa kale, waliotakaswa; kanisa la Mungu, Nazarayo, Pilgrim Holiness, na mengi ya makanisa hayo mazuri ya kale ya utakatifu. Nao walizoea kuimba wimbo:

Ninatembea katika njia kuu nzuri ya kale,
Nikiwaambia kila mahali niendako,
Afadhali niwe Mkristo wa kizamani, Bwana,
Kuliko chochote nijuacho.

⁶⁸ Vyema. Zuri sana. Na halafu walikuwa na mazoea ya kuzungunza juu ya njia kuu ya utakatifu. Sasa, ukisoma juu ya hayo, wanayatoa hayo kutoka katika Isaya, mlango wa 35. Sasa, kama ukiangalia, yeye alisema, “Kutakuwako na njia kuu, na njia.”

⁶⁹ Sasa, *na* ni kiunganishi. Unaona? Njia Kuu, haikuwa ni njia kuu ya utakatifu. “Itakuwa ni njia kuu, *na* njia, na itaitwa, ‘Njia ya utakatifu,’” si njia kuu ya utakatifu. “Njia ya utakatifu!” Na njia ya barabara iko katikati ya barabara. Imetengenezwa namna *hii* ili kwamba maji yatasafisha takataka, pande zote mbili, kuiweka barabara safi. Huninii, kama ukiwa na vidimbwi vidimbwi vinavyosimama barabarani mwako, wakati wote, kama haikutengenezwa ipaswavyo. “Njia” iko katikati ya barabara.

⁷⁰ Sasa, upande *huu*, wakati watu wanapoongolewa, nia zao zimeelekezwa moja kwa moja kwa Kristo. Na kama wao ni wasomi kidogo, wala hawadumu kwenye maombi, watakuwa baridi sana, na wakavu, na waliokakamaa, na wa kawaida. Na halafu kama wao wana wasiwasi kidogo tu, kama usipokuwa mwangalifu, watakuwa washupavu tu na wakati, upande *huu*, unaona, wanaingia katika mihemuko na kila kitu.

⁷¹ Sasa, lakini, Kanisa halisi ni Injili timamu hasa, iliyo katikati kabisa ya barabara. Si baridi wala kavu, wala si kukereketwa. Ni Injili halisi, nzuri, ya kale, yenye joto, ya upendo wa Mungu moyoni, inayopita moja kwa moja katikati ya barabara, ikiita kutoka pande zote mbili. Hiyo ni kweli. Sasa hivyo ndivyo. . . Nanyi mtaipataje hiyo, enyi kanisa? Moja kwa moja kutoka katika Neno, hizo Urimu Thumimu.

⁷² Sasa, Paulo alitaka kuliweka kanisa hili katikati kabisa ya barabara, kwa hiyo alikwenda na akayachunguza kwa Maandiko aliyojua kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, Paulo aliandika sehemu kubwa ya hili Agano Jipya. Mungu alimfanya afanye jambo hilo kwa maana wakati wa Mataifa ulikuwa unakuja. Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, zile Injili nne, walikuwa ni Wayahudi. Lakini Paulo aliandika nyaraka karibu zote.

⁷³ Sasa angalia, basi, tutaanza msingi huu mara moja, mahali alipo, akiliandika, kutoka gerezani. Naye alikuwa amepata ujuzi huu wote. Lakini, kwanza, ujuzi huu ulithibitishwa kwanza, na huu ndio waraka wake muhimu kwa huo. Huu ndio waraka wake

muhimu. Warumi na Waefeso, na kadhalika, zina mahali pao, bali huu ndio waraka muhimu.

⁷⁴ Sasa, mlango wote wa 1, ni, kumwinua Yesu, na kumtenganisha na kuwa nabii. Hicho ndicho kiini kizima cha somo sasa. Nitajaribu kulifikia upesi tu niwezavyo sasa, kusudi tusikae sana. Somo lote, ni, kutenganisha mlango mpya... mpya... Mlango wa 1, ni, kumtenganisha Yesu na nabii yeyote, ama torati yoyote, ama mambo mengine, na kuonyesha Yesu ni Nani. Sasa angalia, “Mungu.” Tunaanza, neno la kwanza, “Mungu.”

Mungu, kwenye za-... ambaye alisema zamani...

Zamani maana yake ni “huko nyuma kabisa,” zamani za kale.

... zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,

⁷⁵ Sasa, unaona, “Mungu, kwa sehemu nyingi, huko nyuma kabisa, alisema na baba zetu katika manabii.” Hivyo ndivyo ilivyombidi kutoa Ujumbe Wake, kupitia nabii Wake.

⁷⁶ Mungu angemtuma nabii Wake kama vile Eliya, Yeremia, Isaya. Na kama utaangalia, kamwe katika historia yote ya dunia, kanisa halijawahi kutoa nabii. Chunguza jambo hilo katika Agano la Kale, Agano Jipya, ama katika siku hizi, katika siku za baadaye. Nionyeshe nabii yeyote aliyewahi kuinuliwa kutoka kanisani katika siku za mwisho. Nionyeshe mmoja aliyewahi kuzuka, kutokea. Pia nionyeshe wakati mmoja ambapo nabii, mtumishi halisi wa Mungu, ambaye mfumo wa kikanisa wa ulimwengu haukumkataa.

⁷⁷ Hebu wazieni tu jambo hilo. Yeremia, Isaya, kote huko nyuma katika Agano la Kale, wanalishutumumu jambo hilo. Yesu alisema, “Mnayapamba makaburi ya manabii na kuyapaka chokaa, nanyi ndio mliowaweka humo.” Hiyo ni kweli.

⁷⁸ Kanisa linaendeleza jambo hilo. Mwangalie Mtakatifu Patrick. Ninyi Wakatoliki mnadai ni wa kwenu. Yeye si Mkatoliki zaidi ya nilivyo mimi. Hiyo ni kweli. Lakini mnadai ni mtu wenu.

⁷⁹ Mwangalie Mtakatifu Francis wa Assisi. Mnadai ni wenu. Yeye si Mkatoliki zaidi ya nilivyo mimi.

⁸⁰ Mwangalie Joan wa Arc. Mlimchoma moto kwenye nguzo, kama mchawi, kwa sababu aliona maono na ni wa kiroho. Mkamchoma moto kwenye nguzo. Na huyo mwanamke akipiga mayowe apate rehema, nao wakamchoma moto kwenye nguzo. Yapata miaka mia moja baadaye, walikuta kwamba yeye alikuwa ni nabii mke. Alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Loo, bila shaka, mlitoa adhabu kubwa: mliichimbua miili ya hao makasisi na kuitupa mtoni.

⁸¹ “Mnayapamba makaburi ya manabii, na kuwaweka mle ndani.” Ni kweli. Kamwe mfumo wa kikanisa haukuwahi kutoa mtu wa Mungu; kamwe haujafanya hivyo, haujafanya hivyo leo, wala kamwe hautafanya hivyo. Dini ya taratibu za kidini kamwe haijawahi kuwa wazo la Mungu.

⁸² Kanisa la zamani sana la kimadhehebu duniani ni kanisa Katoliki; Luther, la pili; ndipo likaja la Zwingli; baada ya la Zwingli, likaja la Kalvin; Kalvin, na kuendelea, Anglikana, Waanglo-Sakson wakifuata, halafu kanisa la Kianglikana; na Mfalme Henry wa Nane, wakati alipopinga, na kadhalika; na kuendelea moja kwa moja hata kwa Methodist ya Wesley, na Wanazarayo, Wapilgrim Holiness; na kushuka chini hadi lile la mwisho, ni la Kipentekoste, yote yaliunda madhehebu. Na Biblia inafundisha dhahiri ya kwamba kanisa Katoliki ni—ni mwanamke mwenye sifa mbaya, na makanisa ya Kiprotestanti na madhehebu yao ni binti zake, Ufunuo 17. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo ni ninii. . .

⁸³ Si hao watu, sasa. Kuna watu wazuri katika makanisa hayo yote; watakatifu, waliookoka. Lakini Mungu haiti watu Wake kwa madhehebu. Yeye huwaita kama watu binafsi. Mungu hushughulika na watu binafsi, iwe wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mprotestanti, na Mkatoliki, ama chochote ulicho. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuja, na aidha ulikusudiwa tangu zamani upate Uzima wa Milele, au alikukusudia kupotea Milele. Si. . .

⁸⁴ Yeye hakutaka kwamba upotee, uangamie. Lakini, Yeye akiwa ni asiye na kikomo, ilibidi ajue mwisho tangu mwanzo, vinginevyo Yeye si Mungu. Kwa hiyo Yesu kamwe hakuja duniani ili kusema tu, “Vema, nitaona endapo mtu fulani atakuwa na huruma. . . Kama nikichukua hatua nife, kwa njia ya kikatili, hao labda watawazia, ‘Vema, mimi. . .’ Ita—itaishawishi mioyo yao, nao wataninii. . .” Mungu haendeshi shughuli Zake namna hiyo.

⁸⁵ Yesu alikuja kwa kusudi moja maalum, hilo ni, kuwaokoa hao ambao Mungu, kabla ya kuwekwa misingi wa ulimwengu, alijua wangeokolewa. Yeye alisema hivyo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo ninii ni. . . “Si katika uweza wa yeye atakaye, wala yeye apigaye mbio; ni Mungu arehemuye.” Paulo alisema jambo hilo. Mtu yule yule hapa.

⁸⁶ Yeye alisema, “Hiyo ndiyo sababu Mungu angeweza kusema, kabla ya Esau ama Yakobo yeyote wao wawili hajazaliwa, Yeye alisema, ‘Ninampenda mmoja na kumchukia huyo mwingine.’” Kabla ya mmojawapo wa wavulana hao hajazaliwa, Mungu alijua ya kwamba Esau alikuwa ni laghai, na alijua ya kwamba Yakobo alikuwa ninii. . . aliipenda haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Kwa hiyo Yeye alijua kuhusu jambo hilo, kabla ulimwengu haujaumbwa. Sasa, tutaona mnamo dakika moja

kwamba Huyu alikuwa ni nani aliyejua jambo hilo. Mlango huu unalo hilo.

Mungu, . . . *alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,*

Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwanawe, . . .

Ati amefanya nini? “Amesema nasi katika siku hizi za mwisho katika Mwanawe.”

⁸⁷ Sasa, ungewazaje basi, kwamba, nabii angekuwa ni mtu wa namna gani? Je! tungekuwa na nabii basi wa siku hizi? Kabisa. Yeye angesema kwa njia hiyo? Hakika. Lakini yeye ambaye . . . Wale manabii wa kale walikuwa ni Roho wa Yesu Kristo.

⁸⁸ Sasa, hebu na tulipate hilo sawasawa, maana sidhani linazama ndani vizuri. Sasa, hii ni kama tu Shule ya Jumapili, kwa hiyo tunataka kupata jambo hili waziwazi. Unaona?

⁸⁹ Angalia. Hebu na tuchukue Roho wa Mungu aliyekuwa katika Musa, kile kikamilifu . . . ni kivuli cha kumtangulia Yesu Kristo. Mifano yote ya Agano la Kale inaonyesha ni kivuli cha msalaba. Musa, alizaliwa akiwa mtoto maalum, akafichwa kwenye manyasi, akaondolewa kwa wazazi wake, na kadhalika, naye alikuwa . . . Yeye alikuwa ni mfalme, ama ki—kiongozi, mtoa sheria, mpatanishi, kuhani. Kila kitu alichokuwa kilikuwa ni kivuli cha Kristo.

⁹⁰ Mwangalie Yusufu, alipendwa na baba yake, akachukiwa na nduguze, na akauzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha. Akatupwa shimoni, akidhaniwa amekufa; akatolewa humo. Katika mateso yake, mnyweshaji aliokolewa, na bucha akapotea; wezi wawili msalabani. Na ndipo wakati alipotoka, aliinuka na akatoka kwenye lile shimo, kisha akaketi kwenye mkono wa kulia wa Farao, taifa lililokuwa kubwa sana kibiashara . . . ta—ta—taifa lililoshinda ulimwengu wote. Wala hakuna mtu angaliweza kumjia Farao wasipopitia kwa Yusufu; Yesu akiketi mkono wa kuume wa Mungu, wala hakuna mtu awezaye kumjia Mungu ila kwa njia ya Kristo. Na wakati Yusufu alipoondoka kwenye kiti hicho cha enzi na akaanza kutoka, watu walitangulia mbele zake, wakipiga makelele ya chereko na kupiga matarumbeta, kupiga tarumbeta, wakisema, “Pigeni goti! Yusufu yuaja.”

⁹¹ Na wakati Yesu atakapokuja, baragumu italia, na kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri. Naam, bwana. Alikuwa ndiye Huyu hapo.

⁹² Na wakati Yusufu alipokufa, aliacha kumbukumbu kwa hao waliokuwa walingojea ukombozi.

⁹³ Niliweka mkono wangu kwenye jeneza hilo la kale, hapa si muda mrefu uliopita, lilikuwa limetengenezwa kwa risasi. Na mwili wake ulipaswa kukaa . . . mifupa yake . . . Kasema,

“Msinzike hapa, kwa kuwa siku moja, Mungu atawazuru.” Yeye alikuwa nabii. “Mungu atawazuru.” Aidha akasema, “Mtakapopanda kwenda kwenye nchi ya ahadi, ichukueni mifupa yangu.”

⁹⁴ Pale, mzee Mwebrania, akiwa na mgongo uliocharazwa na kujaa damu, angeweza kuangalia ndani ya jenezwa hilo na kusema, “Siku moja, tutatoka.”

⁹⁵ Yesu aliacha kumbukumbu, kaburi tupu. Siku moja tutakapoenda kaburini, na wapendwa wetu, na kusikia maskini yale mabonge ya kale, wakati wanaposema, “Majivu kwa majivu, na mavumbi kwa mavumbi, na udongo kwa udongo.” Lakini, ndugu, tunaweza kuangalia ng’ambo ya bahari, kwenye kaburi lililo wazi. Siku moja, tutatoka hapa. Tunaenda nyumbani. Yeye anakuja. Kila kitu kilionyeshwa kwa mfano.

⁹⁶ Mwangalie Daudi, alikataliwa na watu wake mwenyewe, akaondolewa kwenye kiti cha ufalme na watu wake mwenyewe. Akiwa mfalme wa Yerusalemu, alifukuzwa akatolewa Yerusalemu na watu wake mwenyewe. Na alipokuwa akikwea Mlima wa Mizeituni, aliangalia nyuma na kulia. Alikuwa amekataliwa.

⁹⁷ Miaka mia nane tangu wakati huo, Mwana wa Daudi, Mfalme wa Yerusalemu, aliketi kilimani na kulia, maana alikuwa amekataliwa.

⁹⁸ Huyu alikuwa ni Roho wa Kristo katika Daudi. Wote walikuwa wakitangulia kuonyesha msalaba. Hao manabii kule nyuma walinena katika Jina Lake. Waliishi katika Jina Lake. Walitenda mambo katika Jina Lake. Hakika. “Mungu kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alinena na baba zetu kupitia manabii, bali katika siku hii ya mwisho katika Mwanawe.”

⁹⁹ Kwa hiyo manabii na watu wa kiroho, siku hii, ni akiso tu la Kristo. Kule, walisimamia torati, uone. Huku wanasimama, wakiangalia nyuma upande mwingine, kupitia neema.

¹⁰⁰ Hayo yako kwenye Waebrania 11, mlango wa mwisho, mara kwa mara nimeshangazwa na jambo hilo. Katika mlango huo wa mwisho, ile sehemu ya mwisho ya mlango wa 11 wa Waebrania, wakati anapozungumza juu ya Ibrahimu. Ule mlango mashuhuri wa imani, na hapo mwisho, yeye alisema, “Walizunguka-zunguka wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, na wakiwa wahitaji, na kukatwa kwa misumeno. Walizunguka-zunguka, hawana kazi, walichukiwa, na kudharauliwa, na kuteswa. Watu ambao, ulimwengu huu haustahili kuwa na watu kama hao.”

¹⁰¹ Kisha Paulo anasimama na akasema, “Lakini pasipo sisi wao si wakamilifu.” Kwa kuwa waliangalia *wakiutarajia* msalaba tu, na sisi tunaangalia *kupitia* msalaba. Sisi tuna Roho wa Kristo baada ya Huo kufanyika mwili wa kibinadamu na akaishi

miongoni mwetu. Tunakuja hapa kwa Roho Mtakatifu, ambao ni mpango ulio bora zaidi.

¹⁰² Na wakati mwingine ninashangaa yale Ukristo unayotarajia siku hizi. Mhubiri akienda na hema itabidi awe na . . . ama kanisa fulani jipya ama jukumu fulani jipya, anajiita nabii, anaenda pale, na aseme, “Vema, kama watanipa kiasi fulani cha fedha. Kama ninaweza kuwa na gari lililo zuri kuliko yote. Kama wataninii . . . Kama mshahara wangu utaongezwa kila baada ya miezi sita.”

¹⁰³ Inatupasa kuwa na yaliyo bora sana. Inatupasa kuwa na makazi yaliyo bora sana. Inatupasa kuwa na nguo zilizo bora sana. Tutafanyaje tutakaposimama mbele ya hao watu waliozunguka-zunguka, katika ngozi za mbuzi na ngozi za kondoo, hawana mahali pa kulaza vichwa vyao, wakizunguka-zunguka kwenye majangwa? Na mtu fulani anaweza kutudhihaki nasi tuko tayari kuondoka kanisani wala tusirudi huko tena. Kile Ukristo unachohitaji siku hizi. Tunapaswa kujionea aibu.

Ee Mungu, uturehemu.

¹⁰⁴ Katika siku ile, Yeye alisema katika manabii, bali siku hizi kwa Mwanawe. Hilo lilikuwa ni neno la nabii, kule. Hili ni Neno la Mwana, siku hizi. Loo, Jina la Bwana libarikiwe!

¹⁰⁵ Kwa maneno mengine, kama unaangalia kivuli, yaani negatifu, huenda ukakosea. Lakini hii imesafishwa, picha hii ni dhahiri. La wakati ule lilikuwa ni la nabii; hili ni kwa Mwanawe. Lile lilikuwa ni kwa negatifu; hili ni kwa kilicho dhahiri. Amina. Unaona jambo hilo? Hakuna nafasi ya kupoteza. Ni jambo dhahiri, siku hizi katika Mwanawe. Loo, ni ajabu jinsi gani!

*. . . aliyemweka kuwa mrithi . . . (loo, jamani) . . .
mrithi wa yote, . . .*

¹⁰⁶ Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni kuwekwa mamlakani. Loo, sikilizeni. Yeye aliwekwa kwenye mamlaka, Kristo aliwekwa mamlakani, mrithi wa yote. Loo, Ibilisi alijua jambo hilo, tangu bustani ya Edeni, unaona, wakati Ibilisi aliposikia Neno hilo pale siku hiyo, katika hukumu ya watu wale. Lilisema, “Kwa kuwa ulitoka mavumbini; mavumbini utarudi; na Uzao wa huyo mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka.” Uzao ulioahidiwa.

¹⁰⁷ Shetani daima alivizia Uzao huo. Wakati Habili alipozaliwa, yeye alisema, “Ehee, huo hapo ule mzao.” Ndipo akamwua Habili. Mwanawe, Kaini, akamwua Habili. Na mara Habili alipokufa, yeye alisema, “Nimeupata ule mzao.” Akamuuu. Akasema, “Nimeupata.” Lakini, kifo cha Habili, kuzaliwa kwa Sethi kulikuwa ni kufufuka tena. Angalia jinsi walivyofuatana.

¹⁰⁸ Ukoo huo wa Sethi, ukaja, mtu mnyenyekevu, mwenye haki; ukaendelea kupitia kwa Henoko; ukashuka ukaja kwa Nuhu, hata mwisho wa siku zilizotangulia maangamizi ya gharika.

109 Angalia ukoo wa Kaini, ulikuwa wa watu werevu, wenye elimu, sayansi. Je! Biblia haisemi. . . Hivi Yesu hakusema, ya kwamba, “Wana wa ulimwengu huu ni werevu kuliko Wana wa Ufalme”? Angalia upande wa Kaini hata leo hii: werevu, wenye elimu, wenye kushuku, wa kidini sana; unaona, ni wa kidini sana, bali ni wanasayansi, wajenzi, watu mashuhuri.

110 Hebu wachukue watu wakuu. Mwangalie Thomas Edison, watu wengi wakuu. Mwangalie Einstein, bongo za ulimwengu, wanavyoitwa, siku hizi, bongo za ulimwengu. Bali hatujaribu kutumia akili. Tunaacha Nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yetu, na kuangalia kwenye Neno hili, na kuliita hivyo.

111 Madaktari wa madawa, ingawa tunawapongeza kwa yote tuliyo nayo, bali wengi sana wa hao ni wenye kushuku, wasioamini kuna Mungu. Waangalie watu walio werevu, wenye akili siku hizi. Wao wako upande ule mwingine kule, upande wa Kaini.

112 Bali angalia wale walio wanyenyekevu na wapole. Huko hapo kufufuka kwako tena. Loo, Jina la Bwana lisifiwe. Haya basi. Angalia.

. . . yeye alimfanya mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu;

Ni nani aliufanya ulimwengu? Kristo. “Je! Kristo aliufanya ulimwengu?” Naam, bwana. Hebu na twende mbele kidogo tu.

Yeye kwa kuwa ni mng’ao wa utukufu wake na chapa ya uwepo wake, . . .

Ati mng’ao wa utukufu wa nani? Utukufu wa Mungu. Ati chapa ya Uwepo wa Nani? Wa Mungu. Loo, nalipenda jambo hili!

. . . ama chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa neno la . . .

Haya basi. Neno, linalovichukua vitu vyote. Yesu alisema, katika Mathayo 24, “Mbingu na nchi vitapita, bali Maneno yangu hayatapita kamwe.” Yeye anavichukua vitu vyote.

113 Sayansi hujaribu kukishusha Hicho, na kusema, “Ni Kitabu cha kale. Kimefasiriwa.”

114 Hata kanisa Katoliki la Kirumi, Askofu Sheen alisema, “Hicho kimefasiriwa mara nne ama tano mbali mbali, wala hakina thamani sana. Usingeweza kuishi Kwacho kama ungetaka kufanya hivyo.” Lakini anavichukua vyote kwa Neno Lake. Amina. Hivyo ndivyo ninavyowazia juu Yake. Ninaamini Biblia.

. . . kwa neno la uweza wake (kuna nguvu katika Neno), akiisha kufanya utakaso wa dhambi zetu, . . . (angalia hapo) . . . aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;

115 Paulo anajaribu kufanya nini? Anajaribu kuonyesha ya kwamba Mungu alikusudia mambo yote katika Kristo, naye Kristo alikuwa ndiye chapa halisi ya Mungu. Mlango wote mzima uliosalia unashughulika na jinsi Yeye alivyokuwa mkuu kuliko Malaika, mkuu kuliko mamlaka zote. Malaika walimwabudu. Paulo alikuwa akijaribu kumtukuza.

116 Sasa, ninataka kujaribu... kama sitaenda mbali zaidi ya hapa, yaliyosalia ni kumtukuza tu Kristo. Yale Paulo anayosema hapa, kama vile katika mlango wa 11, na yote kuhusu kuzungumza juu ya ulimwengu. Yeye alisema, “Ni—ni Malaika gani Yeye alisema, ‘Wewe ni Mwanangu, leo nimekuzaa?’ Unaona?”

117 “Mwisho wa ulimwengu, wataangamia. Ulimwengu utaangamia. Lakini ninii... Na vitu vyote vya ulimwengu vitaangamia. Yeye atavikunja kama vazi. Vitachakaa, na kubadilika, na kutoweka. ‘Bali Wewe unadumu. Wewe unadumu milele. Wewe ni Mwanangu. Leo nimekuzaa, wala kamwe hutaangamia, ukiketi mkono wa kuume wa Ukuu.’”

Mkono wa kuume una maana gani? Si, eti Mungu ana mkono wa kuume ambao mtu fulani ameketi juu yake. *Mkono wa kuume* unamaanisha “nguvu na mamlaka,” ana mamlaka juu ya kila kitu Mbinguni na duniani. Na Mbingu zote na dunia zimeumbwa na Yeye.

118 Sasa, Jamaa huyu mkuu ni nani, Jamaa huyu mkuu? Kristo. Hapa, Mungu katika Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, si... Ni utatu, bali si utatu wa watu. Ni utatu wa ofisi, za Mungu mmoja.

119 Yeye alikuwa ni Baba akiwaongoza wana wa Israeli. Huo ndio uliokuwa wadhifa Wake, yule Yehova Baba mkuu. Naye aliishi duniani, akaitwa Mwana. Na sasa Yeye anaishi katika Kanisa Lake, akiitwa Roho Mtakatifu. Si Miungu watatu; Mungu mmoja katika ofisi tatu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

Watu wanajaribu kumfanya Yeye ni Miungu watatu mbalimbali, Mungu Baba. Hiyo ndiyo sababu, Wayahudi, usingeweza kamwe... Hutaleta Myahudi jambo hili kamwe, la, hilo hapo. Yeye hawezi. Ana amri, ya kwamba, “Mimi ni Mungu Mmoja.” Kuna Mungu mmoja tu.

120 Huko Afrika wanabatiza kwa njia tatu mbalimbali: wanabatiza mara moja kwa ajili ya Baba, na mara moja kwa ajili ya Mwana, na mara moja kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Ile misheni ya Imani ya Mitume, wao wanabatiza mara tatu, kifudufudi, kwa ajili ya mauti Yake. Kile wanachoita Full Gospel kwenye Pwani ya Magharibi, ama Pwani ya Mashariki, wanabatiza mara tatu kichalichali, walisema Yeye... katika kuzikwa Kwake.

Naye alisema, “Wakati alipokufa, Yeye alianguka mbele.”

¹²¹ Mwingine alisema, “Ngoja. Unamzika mtu kichalichali.” Ni mambo madogo-madogo tu ya kimila ya kufanya jambo, ambapo, wote wawili wamekosea; wote wamekosea, kulingana na Maandiko.

Hii ndiyo Urimu Thumimu. Inatatua jambo hilo.

¹²² Sasa, hapa, hebu tu na tuangalie jambo hilo vizuri na tuone vile—vile linavyoonekana, usiku wa leo. Hili hapa, kama unataka kuliona. Katika miaka yote kama ishirini na mitano ambayo nimekuwa mhudumu. Nimechunguza jambo hilo. Na mara nyingi nimeshangazwa na karama kanisani. Hizo karama ni nini? Unabii, kuna kwa lugha, kufasiriwa kwa lugha, ufunuo wa Kiungu, na kadhalika, zote hizo zinakuja kwa njia ya Kristo.

¹²³ Sasa angalia. Kristo ndiye Kichwa cha mambo yote. Naye ndiye kichwa cha Kanisa. Na je! ulipata kuona almasi kubwa? Almasi kubwa mno iliyokatwa vizuri, ina vipande vidogo vilivyotolewa kwake, vilivyokatwa toka kwake. Kufanya hivyo kunaifanya almasi hiyo kuwa safi. Vipande hivyo ni vya nini? Almasi halisi, jinsi inavyotokea, imechubuliwa; almasi halisi, inapopatikana.

Nilikuwa huko Kimberley. Ninyi, wengi wenu, ambao mmesikia mnaweza kuokota almasi barabarani, hilo ni kweli. Mimi na Billy, na Bw. Bosworth. Rais wa migodi ya almasi huko Kimberley, alitupeleka. . . Alikuwa ndiye bawabu wangu kwenye mkutano kule. Nao walinipeleka huko. Na kutoka tu nje ya. . . Wanazichimba kama, loo, yapata futi elfu moja mia saba chini ya ardhini. Zinatoka, zikiwa jiwe la bluu, kubwa la bluu, kama hili jiwe la bluu mnalopata hapa. Na hao wananchi, wanawashusha futi elfu moja mia saba ardhini, kuzichimbua, wapate kudumisha bei ya juu. Ungeweza kwenda mtoni kule, wameulinda kwa mamia ya maili. Uchukue ndoo mbili za galoni kumi, alisema, na kuzibeba, zimejaa—zimejaa changarawe, na kama ungeweza kufika nyumbani nazo, ungekuwa tajiri wa mamilioni, kungekuwako na almasi nyingi sana ndani yake. Bali inawabidi kuzifanyia kazi na kuzichimbua, wapate kudumisha bei yake juu kwazo.

¹²⁴ Sasa, almasi, inapotokea, ni kipande kikubwa tu, cheroro, kama, mviringo, kipande cha kioo. Kuna almasi ya bluu, almasi nyeusi, zumaridi, na almasi angavu, almasi nyeupe. Lakini inapotoka. . . Ndipo inapotengenezwa na kutumiwa, kuna sehemu ya almasi hiyo ambayo haina budi kupotea. Na haina budi kupoteza vi—vipande vyake vilivyokatwa. Vipande vidogo vinaondolewa, kwa sababu, wakati inapowekwa kwenye nuru ya moja kwa moja, namna *hiyo*, inaifanya kumetameta. Kipande hicho, kinachokifanya kumetameta, ni jinsi inavyokatwa. Inakatwa, inachongwa, na halafu, ikiisha kukatwa, inametameta. Na moja itakuwa na mwako wa

kijanikibichi, hiyo nyingine itakuwa na mwako wa bluu, na labda nyingine, mwako wa zumaridi, na mwako mwekundu. Na miako mbalimbali inatoka kwake, kama rangi ya upinde wa mvua. Wanaiita, “moto ndani ya almasi.”

¹²⁵ Sasa, kila moja ya nuru hizo huwakilisha karama. Lakini ni, ninii tu, Kristo ndiye Almasi. Naye Ndiye aliyekuja, na akachubuliwa, na kujeruhiwa, na kukatwa, apate kujiakisi Mwenyewe kama Nuru kwa ulimwengu. Yeye ndiye ile Almasi Kuu.

¹²⁶ Ungeweza kuwazia, kabla hata hapajawahi kuwa na dunia, kabla hakujakuwako na nuru, kabla hakujakuwako na nyota, kabla hakujakuwako na chochote? Kuna Chemchemi Kuu inayobubujika, ya Roho, na kutoka katika Chemchemi hii ukaja upendo ulio msafi kabisa, kwa kuwa hakukuwako na kitu kingine kingalitoka kwenye hiyo isipokuwa upendo. Sasa, sisi, kile tunachoita upendo, siku hizi, ni upendo uliopotoka. Lakini wakati tu tunapopata tabia, ama kisehemu kidogo cha upendo huo ndani yetu, unabadilisha nia yetu yote.

¹²⁷ Ndipo kutoka hapo kikaja kijito kingine, kutoka kwenye Chemchemi hii kuu, ile Almasi, nacho kiliitwa haki, haki halisi. Sasa, hiyo ndiyo sababu ilitubidi tuwe na torati. Hiyo ndivyo sababu torati haina budi kuwa na hukumu. Hukumu isipoifuata sheria, sheria haifai kitu. Na hukumu ilipotolewa na torati, ambayo huleta mauti, wala hakukuwa na mtu ambaye angaliweza kulipia gharama hiyo ila Mungu Mwenyewe. Naye alilipia hukumu ya mauti yetu, na akachukua dhambi zetu juu ya nafsi Yake, tupate kuwa haki ya Mungu kupitia Kwake.

¹²⁸ Sasa, wakati Nuru hizi kuu zilipotoka, ama miali mikuu ya Roho; upendo, amani, hivyo tu ndivyo vilivyokuwako, Hivyo. Hakukuwako na mateso. Hakukuwako na—na chuki, wala hakukuwa na uovu; hayo yasingetoka katika Chemchemi hii. Huyu alikuwa ni Yehova. Huyu alikuwa ni Yehova Mungu. Na sasa, kama vile wanatheolojia wanavyoiita, thiofania ilitoka katika Hiyo, ambayo iliitwa, Kimaandiko, ile “Logos,” Logos iliyotoka kwa Mungu. Ni vigumu kuelezea, bali ilikuwa ni sehemu ya Mungu.

¹²⁹ Sasa, hivi ndivyo ilivyotukia. Loo, samahani. Ni—ni—ninaingilia tu jambo hili, hili hunipeleka kabisa pale ninapopapenda. Unaona? Logos, na hii Chemchemi kuu, Chemchemi hii kuu ya Roho ambayo haikuwa na mwanzo wala mwisho; Roho huyu mkuu alianza kujiumba, katika ule uumbaji, na ile Logos iliyotoka Kwake ilikuwa ni Mwana wa Mungu. Lilikuwa ndilo umbo pekee la kuonekana ambalo Roho alikuwa nalo. Nalo lilikuwa ni theofania, ambayo maana yake ni mwili, na mwili huo ulikuwa kama wa mwanamume.

130 Musa aliuona wakati ulipopita kwenye . . . karibu—karibu na ule mwamba. Ndipo akauangalia, akasema, “Ulionekana kama mgongo wa mwanamume.”

Ni namna ile ile ya mwili ambao tunapokea tunapokufa hapa. “Kama maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo moja inayongoja tayari.” Ulikuwa ndio Huo. Na huo ulikuwa ndio thiofania ambayo ilikuwa ni Mwana wa Mungu. Huyu Mwana, huyo Logos, alifanyika mwili, kwa kuwa tuliwekwa katika mwili. Na hiyo thiofania, Logos, ilifanyika mwili, hapa miongoni mwetu, nayo haikuwa ni kitu chochote kingine ila mahali pa kuisishi, kwa kuwa Chemchemi hiyo yote ilikaa ndani Yake. Loo, mnaona jambo hilo? Huyu hapo. Huyu alikuwa Ndiye, huyo, katika. . .

131 Angalia hapa. Hebu na tufungue sasa upesi sana katika Waebrania, mlango wa 7, kwa muda kidogo tu juu ya—juu ya neema, Mungu akipenda. Hebu na tuone vile inavyoonekana hapa. Ibrahimu!

Tuna muda gani? Tuna dakika kumi. Vema. Tulipate hili, ndipo tulimalize ijayo, ijayo, ama Jumapili, Bwana akipenda.

132 Ibrahimu alikuwa akirudi kutoka kumpiga mfalme.

Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu, . . .

Ni wangapi wanaojua ni wapi, ni nani, Salemu ilikuwa ni nini? Yerusalemu.

. . .mfalme wa Salemu, mwana mfalme wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;

Sikilizeni.

Ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; (tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena, mfalme wa Salemu, maana yake, yule mfalme wa amani;

Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake; . . .

133 Mfalme mmoja alishuka akaja kutoka Salemu, na akakutana na Ibrahimu akija kutoka kuwapiga wafalme. Na Mfalme huyu hakuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa Uhai. Je! Ibrahimu alikutana na nani? Sasa wazienu. Hakuwa na baba yeyote; hakuwa na mama. Hakuwa kamwe na wakati alipoanza, wala kamwe hana wakati atakapokuwa na mwisho, kwa hiyo Mfalme yuyo huyo wa Salemu hana budi anaishi leo. Amina. Unaona jambo hilo? Ilikuwa ni ule thiofania uliokuwa yule Mwana wa Mungu. Salemu ipi? Ule Yerusalemu ulio Juu, ambao Ibrahimu, akiwa amebarikiwa, alikuwa akiutafuta, kuupata, akijaribu kuupata Mji ambao Mwenye Kuujienga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Alizunguka-zunguka akivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi,

kila mahali, fukara, akizunguka-zunguka, na alikuwa akitafuta Mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Naye alikutana na Mfalme wa huo Salemu, akishuka, naye akampa fungu la kumi la nyara zake zote. Amina. Ndiye Huyo. Loo, Ndugu Graham, huyo alikuwa Ndiye. Huyo alikuwa Ndiye.

Ibrahimu alimwona tena. Siku moja alikuwa ameketi hemani. Akaangalia, wakija kule, naye akaona watu watatu wakija.

¹³⁴ Unajua, kuna kitu fulani tu kuhusu Mkristo, kwamba yeye anamtambua Roho anapomwona. Wakati yeye. . . Yeye anajua hilo kabisa. Kuna kitu fulani tu cha kiroho kuhusu jambo hilo. Mambo ya kiroho yanatambuliwa Kiroho. Unajua. Naam, anaweza tu kujua, kama kweli amezaliwa. “Kondoo Wangu wanajua Sauti Yangu.”

¹³⁵ Naye alijua tu kwamba kulikuwako na jambo fulani. Akatoka mbio. Akasema, “Karibu ndani, Bwana wangu. Karibu uketi. Pumzika kidogo. Nitakuletea kipande cha mkate nikupe mkononi Mwako. Nitakutawadha miguu. Jipumzishe, kisha ukaendeleo na safari Yako, kwa kuwa Wewe—Wewe umekuja kunitembelea.” Huko juu kwenye nchi kame, akishika njia iliyo ngumu, njia ya wachache wa Bwana waliodharauliwa.

Wakati, Lutu alikuwa akiishi katika utajiri, mpwake kule chini, lakini alikuwa akiishi katika dhambi. Kinachosababishwa na utajiri mwingi ni dhambi.

¹³⁶ Kwa hiyo Ibrahimu akawaleta kule, akichukua maji kidogo na kuwatawadha miguu Yao. Akatoka akakimbilia kwenye ndama, na akamchukua ndama mnono kwenye kundi, na kumchinja; akampa mtumishi, kumwandaa. Kisha akasema, “Sara, kanda unga wako.”

Mnajua kukanda, ni nini, kulivyo, kunamaanisha nini. Mnajua, mama alikuwa na kitu cha kale kama namna fulani ya kabari, aliyokuwa nayo kwenye—kwenye pipa la unga. Umewahi kuona kimoja chenye kichungio? Basi wewe uliweka kabari mle ndani, ukakoroga unga, unajua; nao unakuwa mzito namna *hiyo*, na unaukoroga kabisa, hivyo. Nimemwona mama akifanya hivyo, mara nyingi, kabari, tuna kitu kidogo cha duara kilicho na waya wa chekecheke. Angechukua unga huo na kuuchekecha namna *hiyo*, unajua, na kuupepete, namna *hiyo*. Kisha anachukua hiyo kabari na kuuchokoa-chokoa, namna *hiyo*, ili kuushindilia wote. Na hapo ndipo inapotulazimu kushuka kwenda kusaga unga wetu kwenye kinu cha nafaka cha zamani; na misumari mikubwa ya kale, unajua, mzito, ilisaga unga mzuri wa mahindi. Ungeweza kukata magogo kwa msumeno siku nzima, kwa mlo wake.

¹³⁷ Kwa hiyo basi, kasema, “Kanda unga, upesi sana. Kisha uoke keki chache papa hapa mekoni, upesi sana.” Ndipo wakamkamua ng’ombe wakapata maziwa. Ndipo

wakayachukua, wakayasuka, wakapata siagi. Na kisha wakaenda wakamchinja ndama wakachukua nyama, nao wakaikaanga hiyo nyama. Wakachukua siagi ya maziwa, mkate wa unga wa mahindi, kisha wakachukua siagi ya kupaka keki hizo moto moto. Loo, hizo ni tamu hasa. Nao wakaipaka yote kwenye hiyo mikate. Naye akatoa hicho chakula, na akawaandalia hawa Watu watatu.

¹³⁸ Na walipokuwa wakila, walikaza kuelekeza nyuso zao Sodoma. Na baada ya kitambo kidogo, waliamka na wakaanza kwenda zao. Ndipo akasema, Ibrahimu, akasema, “Hutanificha.”

¹³⁹ “Siwezi kukuficha ninaloenda kufanya. Ninashuka kwenda kule. Dhambi za Sodoma zimefika sikioni Mwangu.”

Je! Mtu huyu alikuwa ni nani? Nguo zimejaa mavumbi, na ameketi pale akila nyama ya ndama, na akinywa maziwa ya ng’ombe, na akila keki za unga wa mahindi, na siagi. Jamaa huyu wa ajabu ni nani? Wawili, ama Hao watatu, wameketi pale. Nguo Zake zimejaa mavumbi. Loo, naam, “Tunatoka Nchi ya mbali.” Naam, mbali sana. Na kwa hiyo Yeye akasema. . . Vema, Wao walikuwa ni akina Nani?

¹⁴⁰ Akasema, “Siwezi kumficha Ibrahimu, kwa kuwa yeye ni mrithi wa dunia.” Amina. “Ninawafunulia siri Zangu,” kwa maneno mengine, “kwa wale walio warithi wa dunia.” Hapo ndipo ambapo Kanisa linapaswa kuwa siku hizi. Hiyo ni kweli. Jua Siri za Mungu, ujue jinsi ya kujishikilia, na kutenda, na la kufanya, na jinsi ya kuenenda, na jinsi ya kuishi. Sisi ni warithi wa dunia. Kweli. Yeye anakufunulia Hizo, maana hatakuficha kitu. Hiyo ndiyo sababu tunachunga mambo haya kutimia.

Ulimwengu unasema, “Aha, hilo ni kundi la walokole.” Acha waseme. Mrithi wa dunia anajua mambo haya. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . maana hao wataitwa wana wa Mungu.

Heri hao walio wapole: maana hao watairithi nchi.

Yeye huwajulisha siri Zake, huwafunulia hizo, akiwaonyesha la kufanya na jinsi ya kuishi, wakiyaacha mambo ya ulimwengu; wakienda kitauwa na wakiishi kitauwa, katika ulimwengu huu wa sasa, wakitembea pamoja Naye. Acha ulimwengu useme utakayo.

¹⁴¹ Kwa hiyo akasema, “Siwezi kumficha Ibrahimu siri hii, kwa kuwa nikijua yeye ni mrithi wa nchi. Lakini,” akasema, “Ninashuka kwenda kuuangamiza Sodoma. Ninashuka kwenda huko.”

¹⁴² “Unakwenda kufanya nini, Bwana? Unatoka wapi? Haya yote yana maana gani?”

¹⁴³ Akaja kuona, Yeye akasema, “Na jambo lingine, Ibrahimu, umengojea ahadi hii niliyokupa muda wa miaka ishirini na

mitano. Tayari una vijiatu vyote, vi—vipini na kila kitu, kwa ajili ya mtoto huyu mchanga, miaka ishirini na mitano iliyopita. Ungali umekuwa ukiningojea. Sasa nitakuzuru, wakati huu huu mwakani, kulingana na ninii, wakati ulioahidiwa, mwezi ujawo nitakuwa pamoja nawe.”

144 Naye Sara, huko nyuma hemani. Na Mtu huyu alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, akizungumza na Ibrahimu, namna *hii*. Ndipo Sara akafanya, “A-ha!”

145 Akasema, “Nini kimemfanya Sara acheke?” Ho-ho-ho! Na hilo je! Huko kulikuwa ni kuwasiliana kimawazo kweli, sivyo? “Nini kimemfanya Sara acheke?”

Sara akasema, “La. Sikucheka hata kidogo.”

146 Kasema, “Loo, ndiyo, ulicheka.” Aliogopa. Alikuwa akitetemeka. Huyu alikuwa ni Nani, kujua alichokuwa akifanya nyuma kwenye hema? Huyu ni Mungu yeye yule aliye pamoja nasi siku hizi. Yeye yule. Yeye anajua yote kuhusu jambo hilo. Unaona? Anafunua jambo kadiri tu ulivyo na haja. Unaona?

147 “Unacheka nini?” Unaona, ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Biblia ilisema hivyo, ya kwamba, “Mgongo Wake ulikuwa umeelekezwa hemani.” Lakini, Yeye alijua jambo hilo. “Kwa nini yeye, kule nyuma, anafanya jambo *hili*, unaona?”

Kwa hiyo, Yeye akasema, “Nitakuzuru.”

148 Jamaa huyu wa ajabu ni Nani? Unajua kitu kilichotukia? Alitembea akitoka moja kwa moja pale na akatoweka. Na Biblia ilisema ya kwamba Huyu alikuwa ni Mwenyezi Mungu, Yehova, ile Chemchemi kuu, yule Thiofania, yule Logos.

149 Mhubiri fulani aliniambia, wakati fulani uliopita, akasema, “Ndugu Branham, kwa kweli usingewazia huyo alikuwa ni Mungu, sivyo?”

150 Nikasema, “Biblia ilisema Huyu alikuwa ni Mungu, Elohimu.” Ambaye, Yeye alikuwa ni Mwenyezi Mungu, yule El Shaddai, hiyo ni kweli, Mpaji Nguvu, Yule Mtoshelevu. Amina.

151 Loo, ninajisikia wa kiroho! Wazia jambo hilo, hapa, vile Yeye alivyo sasa. Nitawaonyesha Yeye ni Nani hapa, ndipo mtaona kwamba Mwana ni Nani. Huyu alikuwa ni Yesu, kabla hajapata Jina la kibinadamu, “Yesu.”

152 Alisimama pale kwenye chemchemi ile siku hiyo. Na wote walikuwa wakinywa, unajua, na, “Wakiwa na maji yale yaliyokuwa nyikani,” na vitu kama hivyo. Akasema, “Walikuwa wakila mana.” Kasema, mtu akasema, “Baba zetu walikula mana jangwani, kwa muda wa miaka arobaini.”

153 Akasema, “Nao, kila mmoja wao, amekufa.” Kasema, “Mimi Ndimi Chakula cha Uzima kishukacho kutoka kwa Mungu, Mbinguni. Yeye alaye Chakula hiki hatakufa kamwe.”

154 Kasema, “Vema, baba zetu walinywea Roho, kutoka kwenye Mwamba wa kiroho uliokuwa jangwani, uliowafuata.”

155 Akasema, “Mimi Ndiye ule Mwamba.” Utukufu! Yohana Mtakatifu, mlango wa 6.

“Ona sasa,” wakasema, “ati nini?”

“Naam. Hiyo ni kweli.”

156 “Lo,” mtu mmoja akasema, “Wewe ni ninii. . . Hujapata hata umri wa miaka hamsini bado.” Bila shaka, kazi Yake ilimfanya aonekane mzee kidogo, bali alikuwa na umri wa miaka hamsini tu. Kasema, “Wewe hujapata umri wa zaidi ya miaka hamsini, Nawe unasema umemwona Ibrahimu, ambaye amekufa kwa muda wa miaka mia nane ama mia tisa? Tunajua sasa ya kwamba Wewe ni pepo.”

157 Akasema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Huyu hapo. MIMI NIKO alikuwa ni Nani? Jina la daima kwa vizazi vyote. Huyu alikuwa ni ninii. . . ile Nguzo ya Moto katika kijiti kilichowaka moto, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO.” Huyu hapo, yule Thiofania alikutana hapa, aliyelitwa Mwana wa Mungu, yule MIMI NIKO, yule Yehova.

158 Tomaso akasema, “Bwana, utuonyeshe Baba. Yatutosha.”

159 Kasema, Nimekuwa nanyi muda mrefu namna hii, nanyi hamnijui Mimi?” Kasema, “Unaponiona Mimi, unamwona Baba. Kwa nini unasema, ‘Utuonyeshe, Wewe, Baba?’ Mimi na Baba tu Mmoja. Baba Yangu anakaa ndani Yangu. Mimi ni maskani tu inayoitwa Mwana. Baba anakaa ndani Yangu. Si Mimi ninayefanya kazi hizo, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Yeye ndiye anayefanya hizo kazi, si Mimi.”

160 Sasa, akisimama nyuma kule, tena, Musa alimwona, mgongo Wake, kasema, “Ulionekana kama mgongo wa mwanamume,” Yule Logos aliyetoka kwa Mungu.

161 Basi ni jambo gani lililotukia? Huyu alikuwa ni Mungu. Na sababu ya Yeye kutoka kwenye Logos akafanyika mwili. . . Ni nini? Unaninii vipi. . . Ilitukia nini katika jambo hilo? Dakika tano kabla ya hapo, Yeye alikuwa. . . Alikuwa Logos. Lakini alifanya nini? Alinyosha tu mkono. . .

162 Sasa, miili yetu imefanywa kwa elementi kumi na sita mbalimbali za ulimwengu. Tunajua jambo hilo. Imefanywa kwa potashi, na—na ninii—na kalisiamu kidogo, na—na petroli, na nurulimwengu, na atomi, na kadhalika. Zote zikilundikwa pamoja, na zinaufanya mwili huu, unaotoka kwenye mavumbi ya ardhi. Unakula chakula. Unapokula chakula, ambacho hubadilika kuwa. . . kutoka kwenye mavumbi, nacho kilitoka mavumbini, na ni niniii tu—kinaendelea tu. Mwili wako, tukisema juu ya nyama ya mwili wako, si tofauti na ya farasi, ama na ya ng’ombe, ama chochote kile kingine. Huo ungali ni nyama tu.

163 Na, jamani, unautukuza mwili; bali roho hiyo ina nafsi mle ndani, ndugu yangu. Hiyo ni kweli. Bali mwili wako ni mavumbi tu ya nchi, kama mnyama. Mwili wako si zaidi ya huo wa mnyama. Na kama ukiyatamani mambo ya mwili na mambo unayoona, ukiwatamani wanawake, ukitamani mambo yote haya mbalimbali, huo ungali ni mnyama. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hupaswi kufanya jambo hilo. Roho wa Mungu atakuongoza na kukuweka mahali pa juu kuliko hapo. Hiyo ni kweli kabisa.

164 Sasa, na hapa, Thiofania hii kuu iliyosimama pale. Ni nini? Yule Yehova Mungu mkuu, mnajua alisema nini? Alinyosha tu mkono na akachukua konzi ya atomi, akachukua nuru kidogo, na akajimiminia namna *hii*, akafanya, “Whiu,” mwili, naye akaingia tu ndani yake. Hivyo tu.

165 Kasema, “Njoo hapa, Gabrieli,” yule Malaika mkuu. Akafanya, “Whiu.” “Ingia katika *huo*.”

166 “Njoo hapa, Mikaeli,” yule Malaika anayekaa mkono Wake wa kuume. “Whiu.” Kwa yule. . . “Hebu ingia ndani ya *huo*.”

167 Mungu, na Malaika wawili, alishuka hapa akatembea katika mwili wa kibinadamu, na akanywa maziwa toka kwa ng’ombe, akala siagi kutoka kwenye maziwa, na akala ugali, na akala nyama ya ndama. Malaika wawili pamoja na Mungu. Biblia ilisema hivyo. Huyu ni Melkizedeki, ambaye Ibrahimu alikutana Naye, akija kutoka katika kuwaua wale wafalme. Huyu ni yule Mwana wa Mungu.

168 Nenda mbele, hapa katika Waebrania, wa 7, ilisema, “Bali alifananishwa na Mwana wa Mungu.” Huyu hapo. Alivifanya vitu vyote kwa Yeye. Naye alitoka akatembea moja kwa moja kwenda kule, na akabadilisha tu mavumbi hayo moja kwa moja yakawa mavumbi tena, ndipo akaingia moja kwa moja Utukufuni.

169 Na hao Malaika, mara tu walipowakomboza Lutu na Bibi Lutu, naye akaendelea kuangalia nyuma. Yeye alisema, aliwaambia wasifanye hivyo tena. Nao wakaingia moja kwa moja kurudi ka—katika Uwepo wa Mungu.

170 Sasa, ni tumaini kubwa jinsi gani tulilo nalo, katika Imani hii kubwa tunayotumikia usiku wa leo! Mungu aliye hai, yule Yehova, ile Nguzo ya Moto, iko pamoja nasi. Anajionyesha Mwenyewe katika nguvu, na matendo, na kujitukuza. Aliwaruhusu wapige Picha Yake, Yehova yeye yule. Yule Mwana wa Mungu aliyetoka kwa Mungu, akarudi kwa Mungu, naye anaishi katika Kanisa Lake milele. Huyu hapo.

171 Yeye ameandika majina yetu katika Kitabu Chake, pamoja na kiapo alichopa kwa Yeye Mwenyewe, kwa kuwa hakuna aliye mkubwa awezaye kuapa kwa huyo, ya kwamba atatufua katika siku ya mwisho. “Yeye aulaye Mwili Wangu, na kuinywa

Damu Yangu, yuna Uzima wa Milele, nami nitamfufua katika siku ya mwisho. Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe. Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka hukumuni kuingia Uzimani.”

¹⁷² Yuyo Huyo angeweza tu kunyosha mkono na kunyakua konzi ya kalisiamu na potashi, afanye, “Whiu,” nawe huyo hapo tena. Na jina langu limo kwenye Kitabu Chake. Ho-ho! Hiyo si itakuwa ni siku kweli? Ninajali nini jinsi mabega yangu yanavyozidi kuinama, jinsi ninavyozidi kuzeeka? La hashu. Sina wasiwasi hata kidogo.

¹⁷³ Ndugu Mike, moja ya siku hizi, nakutakia heri, ndugu, wakati hiyo baragumu kuu itakapokuja, sauti hiyo, na Yusufu huyo atajitokeza. Haleluya! Yeye atasema, “Enyi watoto!” “Whiu.” Ninyi hapo mmetokea, tumefanywa katika sura Yake; vijana milele, uzee umepita; magonjwa, shida, huzuni zimetoweka. Utukufu kwa Mungu aliyehai!

¹⁷⁴ Huyo Ndiye anayenena kwa Yeye leo, Mwanawe. “Kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi alisema katika nabii, lakini katika siku hii ya mwisho katika Mwanawe, Kristo Yesu.” Yeye hunena na moyo wa kila mtu ambaye amemwita. Kama umepata kuhisi Sauti Yake ama kumsikia akibisha moyoni mwako, tafadhali usiikatae.

Na tuombe.

¹⁷⁵ Baba wa Mbinguni, usiku wa leo, kwa kuwa sisi tuna furaha sana kujua, kwa kufunguliwa kwa Waraka huu wa Waebrania, jinsi ambavyo Paulo alirudi huko nyuma moja kwa moja katika zile Injili. Asingelichukulia tu kwa kusikiasikia wala kwa ujuzi fulani. Alitaka sisi tujue Kweli ilikuwa ni ipi. Naye alirudi moja kwa moja nyuma katika zile Injili, naye... akarudi kwenye Agano la Kale, ile Injili waliohubiriwa. Naye akaona, kupitia katika Agano la Kale pale, vivuli vyote na mifano. Hiyo ndiyo sababu tunacho Kitabu hiki mashuhuri cha Waebrania usiku wa leo. Nasi tunaona jambo Hilo, Bwana, na tunalipenda. Na kupitia kwenye nyakati nyingi, kimechomwa moto, kimeharibiwa, wamejaribu kukiangamiza, bali kinavuka mawimbini hata hivyo. Kwa maana Wewe ulisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe.”

¹⁷⁶ Ndipo mwenye kushuku angesema, “Vema, ulisema, ‘Paulo alikiandika hiki.’” Si Paulo, bali ni Mungu aliyekuwa ndani ya Paulo; huyo Muumba aliyekuwa ndani ya Paulo.

¹⁷⁷ Kama tu jinsi alivyokuwa ndani ya Daudi, wakati aliposema, “Sitamwacha Mtakatifu Wangu kuona uharibifu, wala sitaiacha nafsi yake katika kuzimu.” Naye Mwana wa Mungu aliyachukua Maneno hayo kutoka kwa nabii huyo, na akashuka akaingia ndani ya moyo wa kuzimu. Na kusema, “Ivunjeni maskani hii, nami nitaifufua katika siku tatu.” Naye

alifanya hivyo, kwa maana Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Nukta moja haiwezi kushindwa. Jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hili, hizi Urimu Thumimu kuu, na kujua ya kwamba ujuzi wetu usiku wa leo, Bwana, unawaka moja kwa moja kwenye Biblia hii hapa! Tumezaliwa mara ya pili, tuna Roho Mtakatifu.

178 Mungu mpenzi, kama kuna mwanamume ama mwanamke ndani hapa usiku wa leo, mvulana ama msichana, ambaye kamwe hajashuhudia jambo hili, wangewezaje kufufuka kama hamna Uzima mle ndani? Loo, wao wanasema, “Nina Uzima.”

179 Lakini Biblia ilisema, “Yeye aishiye katika anasa amekufa akiwa yungali hai.” Unasema una Uzima, bali umekufa. “Unadai,” Biblia ilisema, “kwamba una Uzima, bali umekufa. Unasema wewe ni tajiri wala huna haja ya kitu; wala hujui wewe ni mwenye mashaka, na maskini, na uchi, na kipofu, wala hujui.” Na hiyo ndiyo hali ya makanisa usiku wa leo, Bwana. Jinsi wanavyoyakosa mambo haya makuu, ya thamani.

Kujua ya kwamba yule Yehova Mungu aliye mkuu, Ambaye anaweza tu kutoa kwa . . . Yeye alisema, “Nileteeni hao samaki wadogo.” Ilibidi awachukue wale samaki ku—kufanya kitu fulani nao. Ikionyesha, ya kwamba ufufuo ulibidi uwe ni kitu, kuhusiana nacho. Si kwamba tu aliumba samaki tu, bali aliumba samaki waliopikwa; alioka mikate. Naye aliwalisha watu elfu tano kwa samaki watano wadogo . . . mikate midogo na samaki wawili. Ee Bwana, hayo yalikuwa mikononi Mwake, Naye alikuwa ni Muumba. Bali ilibidi awe na kitu fulani mkononi Mwake.

Mungu, jalia tujiweke mikononi Mwake, usiku wa leo, na kusema, “Ee Mungu, nichukue jinsi nilivyo. Na hapo mwisho wa maisha yangu utakapofika, jalia niende na tumaini hili lililokuwa ndani yangu, nikijua nimezaliwa mara ya pili, na Roho Wako ameshuhudia pamoja nami, na kushuhudia pamoja na roho yangu, ya kwamba Mimi ni Mwanao, ama binti Yako.” Na kwenye siku hiyo ya mwisho, utawafufua. Tujalie, Baba.

180 Na wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, je! kungekuwapo na mtu ungeweza kuinua mkono wako, useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi. Ninataka Mungu anijue mimi wakati. . . kabla sijaondoka humu duniani, ya kwamba Yeye atanijua sana hata Yeye ataliita jina langu. Nitajibu.” Bwana akubariki mwanangu. Mungu akubariki, na wewe; na wewe, bibi. Mtu mwingine? Inua tu mkono wako. Useme, “Niombee, Ndugu Branham.” Hivyo ndivyo tutakavyofanya. Mungu akubariki, bibi mdogo. Hilo ni jema.

181 Sasa, huku kichwa chako kimeinamishwa, ukiomba, nitaimba ubeti mmoja wa wimbo huu.

Usitamani utajiri usio na thamani wa
 ulimwengu huu,
 Ambao huharibika kwa haraka,
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Hayatapita kamwe.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.

¹⁸² Wakati dada anapoupiga sasa, na kichwa chako kimeinamishwa, hebu inua tu mkono wako, useme, “Naam, Bwana, huu hapa wangu”? Utafanya nini? Utaonyesha roho yako, ndani yako, imeamua. “Ninataka mkono Wako, Bwana.” Mungu akubariki, msichana mdogo. “Nitainua mkono wangu.” Mungu akubariki, msichana mdogo, hapa chini. Hilo ni zuri sana, kipenzi. Mungu, unajua, anafurahia kukuona ukifanya hivyo. Waacheni watoto wadogo waje kwangu.”

¹⁸³ “Nataka, Mungu, Wewe uushike mkono wangu. Na katika siku hiyo, ninataka kuwa mkononi Mwako; ili kwamba, utakapoita, nitakuja.” Naam, kama vile ilivyokuwa kwa Lazaro. Mungu akubariki, dada.

Safari yetu itakapomalizika,
 Kama umekuwa mwaminifu kwa Mungu,
 Makazi yako ya Utukufuni yatakuwa mazuri
 na maangavu,
 Nafsi yako iliyojaa shangwe itayaona.

Utafanya nini sasa, basi?

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.

¹⁸⁴ Baba wa Mbinguni, mikono kadha imeinuliwa, katika mkutano huu mdogo, usiku wa leo, kwamba wanataka kushikilia, usiku wa leo, mkono Wako usiobadilika, wa Milele. Tukijua ya kwamba kilichokabidhiwa Kwako . . . Wewe ulisema, “Mimi . . . Wote alionipa Baba Yangu watakuja Kwangu, wala hakuna hata mmoja atakayepotea. Nami nitawafufua katika siku ya mwisho. Hawawezi kuangamia kamwe, hawawezi kamwe kuja hukumuni, bali wana wa Milele, Uzima wa Milele.” Na kuna Uzima mmoja tu wa Milele. Huo hutokana na Mungu, peke yake. Ni Mungu. Nasi tunakuwa sehemu ya Mungu, sana sana hata sisi ni wana na binti za Mungu. Tunapokuwa na Roho wa Mungu ndani yetu, tunawaza kama Mungu. Tunafikiria juu ya haki na utakatifu, nasi tunajaribu kuishi tupate kumpendeza.

¹⁸⁵ Tujalie, Bwana, ya kwamba Uzima wa aina hiyo utamwingia kila mtu aliyeinua mkono wake. Na hao waliopaswa kuinua

mikono yao, wala hawakuinua, ninaomba ya kwamba utakuwa pamoja nao. Tujalie hilo, Baba. Na wakati safari itakapokwisha, maisha yamekwisha, jalia tuingie katika amani kwenye siku hiyo, pamoja Naye, ambapo kamwe hatutazeeka, hatutakuwa kamwe wagonjwa, hatukuwa na shida kamwe. Mpaka wakati huo basi, tudumishe wenye shangwe na furaha, tukimtukuza Yeye, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

¹⁸⁶ Ninyi waamini wote, sasa, hebu na tuinue mikono yetu tu na kuimba pambio hilo.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.

Sasa hebu na tuvumishe [Ndugu Branham anaanza kuuvumisha *Shikilia Mkono wa Mungu Usiobadilika—Mh.*]

¹⁸⁷ Wakati mkifanya hivyo, jirani yako; unasema, “Mungu akubariki, jirani.” Peaneni mikono na mtu anayeketi karibu yako. “Mungu akubariki.” Pande zote mbili sasa. Pande zote mbili, peaneni mikono. “Mungu akubariki, jirani. Mungu awe pamoja nawe.” Jenga matumaini yako kwenye mambo ya Milele.

Doc, najua yapo, ndugu. Ninajua ulikuwa kule, Ndugu Neville, zamani za kale.

Safari hii itakapokwisha,
 Litatukia, moja ya siku hizi.
 Kama tumekuwa waaminifu kwa Mungu,
 Tutamwona Ndugu Seward kule.
 Makazi yako ya Utukufuni yatakuwa yenye
 kung’aa na kung’aa,
 Nafsi yako iliyojaa shangwe itayaona.
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Ninapenda kuabudu huko, baada ya ujumbe.
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika
 Wakati umejaa mabadiliko ya haraka sana,
 Hakuna kitu duniani ambacho kitasimama,
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Shikilia . . .

Hebu na tumtazame Yeye. Yule asiyeonekana miongoni mwetu sasa, na hebu mwabudu tu sasa tunapoimba.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.

Amani! Amani! Amani ya ajabu,
Hebu mwabuduni tu sasa.

Inayoshuka chini . . .

Ujumbe umekwisha. Ni kuabudu.

Tembea juu ya roho yetu milele, naomba,
Katika mawimbi makubwa ya upendo
usiopimika.

Ogeleeni ndani Yake tu.

Amani! Amani! Amani ya ajabu,
Inayoshuka kutoka . . .

Ile Chemchemi kuu, inafunguka.

. . . juu;

Tembea juu ya roho yetu milele, naomba,
Katika mawimbi makubwa ya upendo.

Je! hivi kweli hilo halifanyi jambo fulani?

Amani ya ajabu.
Inayoshuka chini kutoka Juu kwa Baba;
Tembea juu ya roho yetu milele, naomba,
Katika mawimbi makubwa ya upendo
usiopimika.

Je! hivi si kuna kitu fulani kuhusu jambo Hilo, lenye kilindi kabisa na tamu?

¹⁸⁸ Sijui kama kuna mgonjwa anayetaka kupakwa mafuta na kuombewa. Kama yupo, hebu tafuta penye nafasi. Huyu ni yule bibi aliyekuwa kwenye kiti cha magurudumu pale? Mwache tu abaki. Nitakuja, kumwomba. Haitamlazimu kuondoka kitini. Mwingine?

Loo, hivi hampendi tu sehemu hii ya ibada? Ni wangapi wanaojisikia, wanaojua tu ya kwamba Uwepo wa Mungu upo hapa? Huo ndio ninaozungumzia habari zake. Uo huo . . . Unajisikia tu kama . . . Ni wangapi wanaojisikia kana kwamba mngeweza tu kupiga makelele? Sasa hebu tu na tuone. Unajisikia tu kama kitu fulani ndani yako, ungeweza, kinataka kupiga makelele. Unaona?

Ni amani! Amani! Amani ya ajabu,
Inayoshuka chini kutoka kwa Baba huko Juu;
Tembea juu ya roho yangu milele, naomba,
Katika mawimbi makubwa ya upendo
usiopimika.

Niangazie.

¹⁸⁹ Tukiwa katika kuabudu, tutawapaka mafuta wagonjwa sasa, na kuwaomba. Hivi huwezi kuja moja kwa moja huku, mama?

¹⁹⁰ Hii ina maana gani? “Maombi ya imani yatamwoko mgonjwa.” Kila mtu awe katika maombi sasa, vumisheni tu wimbo huo. Wazienu juu ya Yesu akiwaponya wagonjwa. Mpake huyu mama mafuta.



KITABU CHA WAEBRANIA

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org